

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/2203158

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua pepe : ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,

3, Barabara ya Rashid Kawawa,

S.L.P. 5429,

12880, DAR ES SALAAM.

Tanzania

09 Novemba, 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC KUNENGE: STAND MPYA MBEZI LOUIS KUANZA KUTUMIKA RASMI NOVEMBA 30, MAJARIBIO KUANZA NOVEMBA 25.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Abubakar Kunenge amesema Ujenzi wa Stand mpya ya Mabasi ya Mikoani ya Mbezi Louis umefikia 90% na itaanza majaribio ya Kwanza Novemba 25 na kuanza kutumika rasmi Novemba 30.

Kutokana na hilo RC Kunenge ametoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara kuchangamkia fursa zinazopatikana kwenye stendi hiyo ikiwemo fremu za maduka, migahawa, ofisi, huduma za kifedha, supermarket, ofisi za kukata tiketi na hotel ambapo zoezi la kutuma maombi limeanza leo Novemba 09 Hadi Novemba 25.

Aidha RC Kunenge amesema uwepo wa stendi hiyo itaendelea kufungua fursa za maendeleo kwa Wakazi wa Ubungo hivyo amewataka kujiandaa kwa hilo.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM